wanaposhuka Wachina hao, jambo ambalo lilisababisha vicheko zaidi huku kondakta huyo akionyesha kufadhaika na kusema " Leo nimepatikana hata sijui wanashuka wapi, na Kiswahili ndio hawajui".

Ilibidi dereva na baadhi ya abiria wengine kufanya kazi ya ziada ya kuwahoji Wachina, hao mahali wanaposhuka lakini ilikuwa ni kazi ngumu kutokana na kutumia lugha ya Kiswahili lakini hata abiria mmoja alipojaribu kuwauliza kwa Kiingereza bado walionekana kuachwa katika mataa.

Shuhuda wa Asumini, ambae alikuwa ni mmoja kati ya abiria hao alilazimika kufuatilia tukio hilo hadi kufahamu mwisho wake.

Ilibidi gari hiyo ifike mpaka eneo la Darajani, ili kuona kama watashuka na kama ikishindikana waende mpaka Hospitali, na kama huko nako hawatashuka wachukue hatua nyengine.

Lakini Mungu si Athumani, mara gari hiyo ilipofika Darajani, Wachina, hao walishuka na kuwapungia mikono dereva na kondakta huku wakisema maneno ambayo yalionesha kama wanatoa shukrani kwao kwa kuwafikisha salama.

Mara baada ya Wachina, hao kushuka kondakta na dereva wa daladala hiyo walishusha pumzi huku wakionekana kuchoka na kondakta akiapa kutopakia tena watu wa aina hiyo katika gari lake.

SIKUKUU NITATOKA KAMA HIVI AU VIPI!



Annastazia alionekana akienda nyumba ya jirani kuazima simu na kuongea na mtu asiyejulikana na baadaye alitoweka tena ghafla.

Kufuatia hali hiyo, wazazi wake waliitaarifu tena Polisi ambao wamekuwa wakitoa jibu la kuendelea kwa uchunguzi hadi leo bila dalili yoyote ya mafanikio.

Kwa upande wao wazazi wa msichana huyo wamelishushia lawama nzito Jeshi la Polisi sambamba na askari wa Kituo cha Mazizini kwa kauli yao kuwa suala la kutoroshwa msichana sio kesi kubwa ya kwenda mahakamani.

Wazazi hao wameliambia Asumini kuwa walitaka mtoto wao apelekwe Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja akapimwe kujua iwapo amefanyiwa kitendo cha ngono au kuambukizwa maradhi na mwanamume huyo lakini katika hali isiyotarajiwa askari hao walikataa na kudai kuwa hapakuwa na askari wa kike wa kumpeleka.

"Tunashangazwa na kauli za Polisi kuwa eti kutoroshwa sio kesi ya kufikishwa mahakamani kwa vile inazungumzika wakati aliyetoroshwa ni msichana wa miaka 16 aliye huko chini ya dhamana ya wazazi wake, sisi tunaona hatukutendewa haki na ndio maana tumekuiteni hapa waandishi mtusaidie", walisema kwa uchungu wazazi hao.

Akizungumzia kadhia hiyo Padri Peter Caaver Minja wa Kanisa Katoliki Zanzibar akiwa ni mlezi wa waumini wa Kikristo, alisema baada ya kuelezwa mkasa huo alifika Kituo cha Polisi Mazizini, kisha kuonana na Kamanda wa Polisi Mkoa (RPC) wa Mjini Magharibi Bakari Khatib Shaaban na Mkuu wa Upelelezi Mjini (RCO) Bw. Said Marekano waliosema kesi hiyo inafanyiwa uchunguzi.

"Mimi sioni sababu ya Polisi kusema wanafanya uchunguzi wakati vielelezo vyote walivipata, msichana walimkuta nyumbani kwa Salum na mizigo yake waliikuta lakini waliamua kuivuruga kesi hiyo kwa makusudi", alisikitika Padri Minja.

Aliongeza kwa kusema kuwa msichana huyo bado anasoma lakini Polisi haioni umuhimu wa kumuokoa mtoto huyo ili aendelee na masomo yake ambayo ndio dira na muongozo wa maisha yake.

Aliyaomba Mashirika yanayosimamia haki za watoto nchini kuingilia kati kesi hiyo baada ya Jeshi la Polisi kushindwa kutekeleza wajibu wake.

Padri huyo ameeleza hofu yake juu ya msichana huyo kusilimishwa kwa nguvu kwani hata wazazi wa Salum nao wanamuunga mkono mtoto wao kwa kitendo hicho cha kumtorosha msichana huyo kinyume na sheria.

Hadi timu ya waandishi wa habari hizi wanaingia mitamboni bado suluhisho la sakata hilo halijapatiwa ufumbuzi huku wakisubiriwa Jeshi la Polisi kukamilisha uchunguzi wao.

# Matoroli 350 yapigwa mnada kuondoa kero barabarani

Na: Edwin Soko, Mwanza

MAHAKAMA jijini Mwanza imeiamuru Halmashauri ya jiji la Mwanza kuyauza matoroli yapatayo 350 yaliyokuwa yakifanya biashara kinyume na sheria ya jiji na kutoonekana wamiliki wake baada ya kukamatwa na jiji.

Hakimu wa mahakama ya mwanzo Wilaya ya Nyamagana Leonard Ndolezi alitoa hukumu hiyo baada ya kuridhika na upande wa mashitaka ulioendeshwa na mwendesha mashitaka wa jiji Bwambo Macksoud na kusema kuwa wamiliki wa matoroli hayo wameshindwa kuyafuata.

Hivyo mahakama yake imeridhia kutoa amri ya kuuzwa kwa matoroli hayo kwa mnada kwa kuwa hayana mwenyewe aliyejitokeza.

Kwa mujibu wa hakimu huyo, uamuzi huo unafuatia vifungu halali vya sheria mbadala za mahakama za kutotokea mmiliki wa mali zinazokamatwa.

Halmashauri ya jiji imekuwa ikipambana na wafanyabiashara wa matoroli, ambao wamekuwa wakivunja sheria ya kutoendesha matoroli yao katika barabara zilizokatazwa zikiwemo barabara za Nyerere, Kenyatta, Makongoro, Liberty, Rwagasore na Pamba.

Barabara hizo zimekuwa na msongamano mkubwa wa magari pamoja na waenda kwa miguu, ambapo upitishaji wa matoroli katika barabara hizo unadaiwa kuiwa ni chanzo cha ajali nyingi mkoani hapa.

Kufuatia hali hiyo Halmashauri ya jiji imekuwa ikiendesha operesheni kabambe ya kuyashika matoroli yanayokwenda kinyume na sheria hiyo na kuyafungulia mashataka mahakamani.

Hata hivyo, mara nyingi wafanyabiashara wa matoroli hukimbia na kuyaacha matoroli yao yakichukuliwa na Halmashauri ya jiji na pia mashitaka yanapofika mahakamani hawajitokezi na kuamua kuyatelekeza na kusababisha mrundikano mkubwa wa matoroli hali inayopelekea mahakama kutoa amri ya kuuza .